

ROHO MTAKATIFU:

KUTENDA KAZI NYUMA YA PAZIA

A Kazi zilizojificha za Roho Mtakatifu:

❖ Kazi ya siri ya Roho Mtakatifu.

- Akiongea na Nikodemu, Yesu alilinganisha kazi ya Roho mtakatifu na upepo (Yohana 3:5-8).
 - (a) “Huvuma anakopenda”. Hakuna awezaye kumtawala. Hufanya mapenzi yake kwa ufanisi kwa njia iliyo ya siri kabisa.
 - (b) “Unasikia sauti yake”. Japo hatuwezi kumuona, kazi yake ni Dhahiri. Tunaona matokeo ya kazi yake ndani ya watu.
- Anapovuma kwetu (mifupa mikavu), tunapokea uhai mpya wa kiroho.

❖ Kazi yake katika uumbaji.

- Alikuwa akiruka juu ya maji kama tai juu ya makinda wake akiwalinda (Kumbukumbu 32:11). Roho mtakatifu alikuwepo wakati wa uumbaji.
- Roho mtakatifu alikuwa muhusika wa pili akisaidia kazi ya Baba (Mwanzo 1:1) na Mwana (Wakolosai 1:16; Waebrania 1:2).
- Alikuwepo wakati binadamu anaumbwa (“na tumfanye”) na ni muhusika mkuu katika kuifanya dunia upya.

❖ Kazi yake inayoelezea mpango wa wokovu.

- Roho Mtakatifu alitoa karama kwa Bezaleli kufanya ustadi uliohitajika pamoja na ujuzi na uzuri (Kutoka 31:4-5).

B Kazi iliyojificha nyuma ya Yesu.

❖ Kumtukuza Yesu. Yohana 15:26; 16:14.

- Je Roho mtakatifu anamtukuza Yesu kwa jinsi gani?
- Roho mtakatifu hujificha nyuma ya Yesu. Kazi yake ni kutuvuta kwa Yesu na kazi yake ikomboayo.
- Tunamvuta kila mmoja kwa Yesu kama afanyavyo roho mtakatifu, na si kuwavuta kwetu, (wala si kwa Roho mtakatifu).

❖ Kumfanyia kazi Yesu.

- Roho mtakatifu alifanya jukumu la muhimu katika Maisha ya Yesu.
 - (a) Aliwezesha Yesu kufanyika mwili (Luka 1:35); Alimtia mafuta kwa ajili ya utume wake (Luka 3:22); Alimsaidia wakati wa majaribu (Luka 4:1, 14); Alimsaidia katika kazi yake ya kukomboa (Ebr 9:14); Aliwezesha kufufuka kwa Yesu (1 Petro 3:18).
- Roho Mtakatifu anaelendee kufanya kazi kwa ajili ya Yesu katika Maisha ya kila mmoja wetu.
 - (a) Kwa kutumia maandiko hutufundisha habari za Yesu; Anatuongoza katika mahusiano na Yesu yanayookoa; Huzalisha tabia ya Yesu ndani yetu; Hutupatia nguvu ili tuweza kuishi kama Yesu’.